TANGAZO LA SERIKALI Na.1106 la tarehe 27/12/2024

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 16(1))*

SHERIA NDOGO YA USHURU WA STENDI NA MAEGESHO YA HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA YA MWAKA 2024

Jina

**1.** Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ushuru wa Stendi na Maegesho ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa ya Mwaka 2024.

Matumizi

**2.** Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa.

Tafsiri

**3.** Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"ada" maana yake ni malipo yanayolipwa Halmashauri kwa ajili ya kibali cha kuegesha chombo cha usafiri;

"afisa mwidhiniwa" maana yake ni afisa aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"gari" maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirisha abiria au mizigo kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine isipokuwa mikokoteni, baiskeli na wanyama wanaotumika kubeba watu au mizigo;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa,

"kituo cha basi" maana yake ni kituo cha basi kilichoidhinishwa na Halmashauri ambapo mabasi

yanatoa huduma ya kushusha na kupakia abiria na mizigo;

"maegesho" maana yake ni sehemu iliyotengwa au iliyoidhinishwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha magari;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa au afisa aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mmiliki" maana yake ni mwenye gari na inajumuisha dereva au kondakta anayetumia gari;

"stendi kuu" maana yake ni eneo lililoidhinishwa na Halmashauri ambapo magari yanayotoa huduma ya usafiri kwa umma kuelekea mikoani na maeneo yaliyo ndani na nje ya Halmashauri huanzia na kumalizia safari;

"wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi cha watu, kampuni au taasisi iliyoingia mkataba kutekeleza jukumu lolote chini ya Sheria Ndogo hii kwa niaba ya Halmashauri.

Wajibu wa muegeshaji

**4.** Itakuwa ni wajibu wa muegeshaji wa chombo cha usafiri kufuata masharti yaliyowekwa katika Sheria Ndogo hii.

Wajibu wa mmiliki wa magari ya abiria na mizigo

**5.** Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa magari ya abiria na mizigo yanayotoka au kwenda mikoani na maeneo yaliyo ndani na nje ya Halmashauri, kuingia katika eneo lililotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria na mizigo.

Wajibu wa Halmashauri

**6.** Halmashauri itakuwa na wajibu wa kusimamia maegesho yote yatakayoanzishwa katika maeneo yote ndani ya Halmashauri na kuhakikisha inasimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii.

Maeneo ya maegesho

**7.**-(1) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kutenga eneo lolote la Halmashauri kwa madhumuni ya maegesho ya magari.

(2) Halmashauri itabainisha idadi ya magari yanayotakiwa kuegeshwa katika eneo lililotengwa kwa ajili ya maegesho.

(3) Halmashauri au wakala anaweza kuainisha baadhi ya maeneo katika vijiji kuwa ni sehemu ya maegesho yaliyotengwa.

(4) Halmashauri itatenga maeneo maalumu ya maegesho yatakayotumiwa na pikipiki na bajaji kwa ajili ya biashara na baiskeli.

Ada ya kibali

**8.**-(1) Kila mmiliki wa chombo cha usafiri cha biashara ambaye anataka kuegesha chombo chake katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya maegesho kwa vyombo vya biashara, atatakiwa kusajili chombo chake na kupewa kibali.

(2) Kila mmiliki wa chombo cha usafiri cha biashara atatakiwa kulipa ada ya kibali ambacho kitamuwezesha kuegesha chombo chake kwa muda na utaratibu utakaowekwa na Halmashauri kama inavyoelekezwa katika Jedwali la Kwanza.

(3) Itakuwa ni marufuku kwa mmiliki yeyote wa chombo cha usafiri cha biashara kuegesha chombo chake katika maegesho yaliyotengwa kwa ajili ya kuegesha vyombo vya biashara bila kuwa na kibali cha kuegesha katika maeneo hayo kutoka Halmashauri.

(4) Mtu yeyote atapaswa kuegesha chombo chake cha usafiri katika maeneo maalumu yaliyotengwa kwa ajili ya maegesho kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Usimamizi wa kituo cha mabasi

**9.**-(1) Itakuwa ni marufuku kwa basi lolote kushusha au kupakia abiria katika eneo lolote la Halmashauri isipokuwa kwenye maeneo yaliyoainishwa kuwa vituo vya mabasi.

(2) Mabasi yote yanatakiwa kuanza safari zake katika vituo vya mabasi vilivyoainishwa na Halmashauri, isipokuwa kwa kibali maalum kutoka Halmashauri.

(3) Mabasi yote yanayofanya safari za ndani ya eneo la Halmashauri yatatakiwa kusimama katika kituo cha mabasi kwa lengo la kushusha au kupakia abiria kwa

*Tangazo la serikali Na.1106 (linaendelea)*

muda usiozidi dakika tano, isipokuwa kwa kituo cha kuanzia na kumalizia safari.

(4) Itakuwa ni marufuku kwa mmiliki wa basi au gari la aina nyingine kufanya matengenezo ndani ya kituo cha basi au katika eneo lililotengwa kwa ajili ya maegesho.

(5) Bila kuathiri masharti mengine ya Sheria Ndogo hii, Halmashauri itakuwa na uwezo wa kutangaza au kutenga eneo lolote kuwa kituo cha mabasi au maegesho kama itakavyoona inafaa.

Ushuru wa maegesho

**10.-(**1) Halmashauri itatoza ushuru kutoka kwa kila mmiliki wa gari lililoegeshwa katika sehemu za maegesho au kituo cha mabasi kwa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

(2) Ushuru wa maegesho unaweza kulipwa kwa saa, siku, mwezi au mwaka.

(3) Mmiliki wa gari atakayelipia ushuru wa maegesho kwa siku, mwezi au kwa mwaka ataruhusiwa kuegesha gari lake katika eneo lolote lililotengwa kwa ajili ya maegesho kwa muda aliolipia bila kudaiwa tena.

Maegesho maalum

**11**.-(1) Mtu yeyote atakayehitaji kupangiwa maegesho binafsi atawasilisha maombi kwa Halmashauri au Wakala.

(2) Baada ya maombi kukubaliwa, mwombaji atawajibika kulipa ushuru wa maegesho yaliyotengwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili na ataruhusiwa kutumia sehemu hiyo peke yake bila kuingiliwa.

(3) Mtu aliyetengewa eneo kwa ajili ya maegesho binafsi atalipia ushuru wa maegesho endapo atatumia maegesho tofauti na eneo alilotengewa.

Ushuru wa stendi

**12.-(**1) Halmashauri itatoza ushuru wa stendi kwa magari yote yanayoingia katika Stendi Kuu ya mabasi na maeneo mengine yaliyotengwa kwa matumizi ya stendi kwa namna na kiasi kilichoainishwa katika Jedwali la Tatu.

(2) Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa gari au chombo chochote cha usafiri kinachotumia stendi kuu au

eneo lingine linalotumika kama stendi kulipa ushuru wa stendi.

(3) Ushuru wa stendi utalipwa kila gari linapotoka kituoni kuanza au kuendelea na safari zake.

Ushuru wa kulaza gari

**13.-(**1) Halmashauri itatoza ushuru wa kulaza gari stendi au katika eneo lingine lililotengwa kwa matumizi hayo.

(2) Ushuru wa kulaza gari utatozwa kwa kila gari lililolazwa stendi au eneo lililotengwa kwa siku kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Nne .

Gari lililotelekezwa

**14.-(**1) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuegesha gari zaidi ya muda aliolipia ushuru.

(2) Mtu yeyote atakayekiuka kanuni ndogo ya (1) atahesabika kuwa ametelekeza gari na Halmashauri au Wakala anaweza kulifunga gari hilo kwa minyororo hadi hapo mtu huyo atakapolipa ushuru anaodaiwa pamoja na faini.

(3) Gari ambalo litakuwa limefungwa minyororo zaidi ya saa mbili bila kulipiwa ushuru pamoja na faini litavutwa na kupelekwa kwenye eneo litakaloainishwa na Halmashauri na gharama za kulivuta zitakuwa juu ya mmiliki.

(4) Mmiliki wa gari ambalo litavutwa na kuhifadhiwa na Halmashauri ataruhusiwa kuchukua gari baada ya kulipa ushuru unaodaiwa, gharama ya utunzaji, gharama za uvutaji na gharama nyingine ambazo kwa namna moja au nyingine Halmashauri au Wakala atakuwa amegharimia na mmiliki atapewa gari hilo baada ya kutoa uthibitisho wa umiliki wa gari.

(5) Gharama ya utunzaji wa gari itakuwa ni shilingi elfu thelathini kwa siku.

Zuio la kuegesha gari.

**15.** Halmashauri inaweza kuzuia maegesho ya magari katika sehemu yoyote kwa kuweka alama “hakuna kuegesha hapa” au “no parking” kwa sababu zifuatazo:

(a) kurahisisha mzunguko wa magari;

(b) ujenzi au ubomoaji unafanyika katika eneo husika; na

*Tangazo la serikali Na.1106 (linaendelea)*

(c) ikiwa magari kuegeshwa katika sehemu hiyo kutakwamisha shughuli inayofanyika kwa wakati huo.

Magari yaliyosamehewa kulipa ushuru

**16**.-(1) Magari yafuatayo yamesamehewa kulipa ushuru wa maegesho chini ya Sheria Ndogo hii:

(a) magari yote ya mabalozi na wanadiplomasia;
(b) magari ya kubebea wagonjwa;
(c) magari ya Serikali;
(d) magari ya Jeshi;
(e) magari ya Zimamoto; na
(f) magari yote yanayotumika kwa ajili ya usafi katika eneo la Halmashauri.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Halmashauri inaweza kusamehe gari lingine lolote kulipa ushuru wa maegesho iwapo itaridhika na sababu za mwombaji na msamaha huo utatolewa kwa kibali maalum kutoka kwa Mkurugenzi au Afisa Mwidhiniwa.

Makosa

**17.** Mtu yeyote anatenda kosa endapo-

(a) atashindwa kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;
(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru;
(c) atamzuia Mkurugenzi, afisa mwidhiniwa au wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;
(d) atashindwa, atadharau, atakaidi au kukataa kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kuhusiana na ulipaji wa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hii;
(e) ataegesha gari, pikipiki au bajaji bila kulipa ushuru wa maegesho;
(f) ataegesha gari, pikipiki au bajaji katika eneo lisiloruhusiwa;
(g) ataegesha gari nje ya mstari uliochorwa kuainisha eneo la kuegesha gari;
(h) ataosha gari, pikipiki au bajaji kwenye maegesho;

(i) atafanya matengenezo ya gari, pikipiki au bajaji kwenye kituo cha basi au kwenye eneo la maegesho; au

(j) ataegesha vibaya na kuzuia magari mengine kuegeshwa au kutoka kwenye eneo la maegesho.

(2) Wakala aliyeteuliwa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii atatenda kosa endapo-

(a) atatumia nyaraka za kughushi kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa ada au ushuru ndani ya Halmashauri;

(b) atashindwa kutoa taarifa au atatoa taarifa za uongo Halmashauri kuhusu bidhaa au huduma zinazotakiwa kulipiwa ada au ushuru;

(c) hatawasilisha au atawasilisha kwa kuchelewa makusanyo ya ada au ushuru Halmashauri kulingana na muda aliopewa kwa mujibu wa mkataba; au

(d) atashindwa kutunza kumbukumbu sahihi za malipo ya ada au ushuru.

Adhabu

**18**.-(1) Mtu atakayepatikana na hatia kwa kutenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini na isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichopungua miezi sita na kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote.

(2) Endapo mtu aliyepatikana na hatia ni wakala, pamoja na adhabu iliyoainishwa katika kanuni ndogo ya (1) atalipa Halmashauri kiasi cha pesa alizopaswa kulipa au zilizopaswa kulipwa na mlipa ada au ushuru.

Kufifilisha kosa

**19**. Mkurugenzi anaweza kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii kiasi kisichozidi shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kujaza fomu maalumu kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Tano.

*Tangazo la serikali Na.1106 (linaendelea)*

## JEDWALI LA KWANZA

*(Limetenegenezwa chini ya kanuni ya 8(2)*

ADA YA KIBALI

| Na. | Aina ya Gari | Kiasi cha Ada |
|---|---|---|
| i. | Teksi | 7,500/= |
| ii. | Gari dogo la mizigo | 6,500/= |
| iii. | Lori kuanzia chini ya tani 5 | 8,000/= |
| iv. | Lori kuanzia tani 5 hadi tani 10 | 10,000/= |
| v. | Lori zaidi ya tani 10 | 15,000/= |
| vi. | Pick up | 5,000/= |
| vii. | Aina nyingine za magari | 10,000/= |
| viii. | Pikipiki ya matairi mawili | 5,000/= |
| ix. | Pikipiki ya matairi matatu/Bajaji | 5,000/= |

## JEDWALI LA PILI

*(Limetenegezwa chini ya kanuuni ya 10(1) na 11(2))*

USHURU WA MAEGESHO

| Na. | Aina ya Gari | Kiasi cha ushuru kwa saa | Kiasi cha ushuru kwa siku | Kiasi cha ushuru kwa mwezi | Egesho lililotengwa kwa mwaka |
|---|---|---|---|---|---|
| i. | Teksi | 200/= | 1,000/= | 20,000/= | 200,000/= |
| ii. | Gari dogo | 200/= | 1,000/= | 20,000/= | 200,000/= |
| iii. | Lori kuanzia chini ya tani 5 | 300/= | 2,000/= | 50,000/= | 500,000/= |
| iv. | Lori kuanzia tani 5 hadi tani 10 | 400/= | 4,000/= | 100,000/= | 1,000,000/= |
| v. | Lori zaidi ya tani 10 | 500/= | 5,000/= | 130,000/= | 1,300,000/= |
| vi. | Pick up | 200/= | 1,000/= | 20,000/= | 200,000/= |
| vii. | Aina nyingine za magari | 200/= | 1,000/= | 20,000/= | 200,000/= |
| viii. | Pikipiki ya matairi mawili | 100/= | 100/= | 3,000/= | 36,000/= |
| ix. | Pikipiki ya matairi matatu | 100/= | 100/= | 3,000/= | 36,000/= |
| x. | Magari mengine ambayo hayakutajwa | 200/= | 1,000/= | 20,000/= | 200,000/= |

*Tangazo la serikali Na.1106 (linaendelea)*

______________

JEDWALI LA TATU

______________

*(Limetenegezwa chini ya kanuni ya 12(1))*

USHURU WA MAGARI YANAYOINGIA STENDI

| Na. | Aina ya Gari | Kiasi cha ushuru kwa safari moja (Tripu) |
|---|---|---|
| i. | Teksi | 500/= |
| ii. | Bajaji | 300/= |
| iii. | Pikipiki | 200/= |
| iv. | Basi la abiria kuanzua 5-15. | 500/= |
| v. | Basi la abiria chini ya 25 | 1,000/= |
| vi. | Basi la abiria kuanzia 26-65 | 3,000/= |
| vii. | Gari dogo la mizigo | 500/= |
| viii. | Gari kubwa la mizigo | 2,000/= |
| ix. | Magari mengineyo madogo | 500/= |
| x. | Magari mengineyo makubwa | 2,000/= |
| xi. | Magari mengine ambayo hayakutajwa | 2,000/= |

______________

JEDWALI LA NNE

______________

*(Limetenegezwa chini ya kanuni ya 13(2))*

USHURU WA KULAZA MAGARI

| Na. | Aina ya Gari |
|---|---|
| i. | Basi la abiria zaidi ya 40. |
| ii. | Basi la abiria chini ya 40 |
| iii. | Basi la abiria chini ya 20 |
| iv. | Teksi |
| v. | Gari dogo la kawaida |
| vi. | Pick up/ Station Wagon |
| vii. | Guta |
| viii. | Pikipiki ya matairi mawili |
| ix. | Pikipiki ya matairi matatu |
| x. | Gari la mizigo chini ya tani 5 |
| xi. | Gari la mizigo kuanzia tani 5 hadi 10 |
| xii. | Gari la mizigo zaidi ya tani 10 |
| xiii. | Magari mengineyo madogo |
| xiv. | Magari mengineyo makubwa |
| xv. | Magari mengine ambayo hayakutajwa |

*Tangazo la serikali Na.1106 (linaendelea)*

______________

JEDWALI LA TANO

______________

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 19)*

FOMU YA KUFIFILISHA KOSA

Mimi …………………………………………… NAKIRI KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ………………………….ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Wilaya ya Kilwa, kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi ……. mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kanuni ya …… ya Sheria Ndogo ya Ushuru wa Stendi na Maegesho ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa ya Mwaka 2024.

NAKUBALI kulipa ada au ushuru ninaodaiwa kwa kiasi cha shilingi ................ pamoja na faini ya kufifilisha kosa kwa kiasi cha shilingi ..................

NATHIBITISHA KWAMBA, maelezo niliyotoa hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa MIMI MWENYEWE na kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.

Leo hii tarehe………….ya mwezi…………..… mwaka 20…………….
Jina……………………………….....
Saini………........……………….......

MBELE YA MKURUGENZI

Jina:…………………......................................
Saini:…………………..…..............................
Tarehe:..............................................................

*Tangazo la serikali Na.1106 (linaendelea)*

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa imegongwa kwenye Sheria ndgo hizo kufuatia azimio lililopitishwa katika Mkutano mkuu wa baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya kilwauliofanyika tartehe 9/11/2023 na kushuhudiwa Lakiri hiyo ikigongwa mbele ya:-

HANAN M. BAFAGHI,
*Mkurugenzi Mtendaji,*
*Halmashauri ya wilaya,*
*Kilwa*

MHE. ISSA B. MATEKA,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya wilaya,*
*Kilwa*

L.S

**NAKUBALI**,

Dodoma,
29 Oktoba, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI*